**MUHULA WA PILI 2023**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI (102/2)**
**KIDATO CHA TATU (3)**
**MUDA: SAA 2 ½**

**Maagizo**

Jibu maswali yote

Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali

Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili

Kwa matumizi yam tahini pekee

| SEHEMU | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| | 15 | |
| | 15 | |
| | 40 | |
| | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

## 1.UFAHAMU (alama 15)

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Aibu kubwa ya taifa kushindwa kukabiliana na tatizo sugu la ajali barabarani bado inaendelea.Licha ya matumizi ya vidhibiti mwendo na kanda za usalama,ajali za barabarani zinaangamiza idadi kubwa ya watu kila mwaka,wakiwemo viongozi na watu mashuhuri .

Miongoni mwa sababu ambazo zinaleta maafa barabarani ni pamoja na uendeshaji kasi kupita kiasi inavyotakikana ,yaani kuika masharti yaliowekwa na wizara ya uchukuzi .Madereva wengi hung'oa vidhibiti mwendo vilivyowekwa ,hawarekebishi mikanda ya usalama ,wala hawapeleki magari yao kwa ukaguzi mara kwa mara kama inavyopaswa ,kutelekeleza kanuni zilizowekwa kwa hivyo hutegemea hongo kuwa barabarani.Fauka ya hayo,madereva wa malori na matrela mara nyingi huendesha magari yao wakiwa walevi.Dawa za kulevya kama vile miraa na bangi hutumiwa sana na watu hawa, na matokeo yake huwa ajali mbaya.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Hata hivyo ,lawama haiwezi kuelekezewa madereva pekee.Ukiangazia barabara nchini utapata kuwa bararabara nyingi nchini Kenya haziko katika hali nzuri.Zile za lami zimekuwa na mashimo makubwa ambapo mvua ikinyesha hufanya vidimbwi mithili ya machimbo ya madini yaliojaa maji baada ya kuachwa wazi.Aidha, barabara zisizokuwa za lami zimeharibika kiasi kwamba ni vigumu kuzitofauisha na njia za ng'ombe kwenye maeneo kame. Kinachohitajika ni serikali kuzifanyia ukarabati ili kuzirudisha katika kiwango ambacho zitaweza kufaa.

Wananchi pia inafaa waelimishwe ili wasikubali kuingia kwenye magari ambayo tayari yamejaa kupita kiasi.Hili litawasaidia wananchi wenyewe kudumisha usalama wao barabarani .Pia inafaa watambue ya kwamba wana jukumu la kuwaarifu walinda usalama endapo dereva ameendesha kwa kasi sana kuliko ile ya kilomita 80 kwa saa iliyokubaliwa.

Inafahamika kuwa baadhi ya maafisa wa usalama ni wafisadi ,hivyo basi huchangia katika kuongeza idadi ya vifo barabarani. Katika vita vya ufisadi na ajali za barabrani, ni mwananchi mwenyewe ambaye atawezesha kukomesha hali hii.Kwa mfano ,afisa wa usalama akipatikana akichukua hongo ,yeye pamoja na yule aliyetoa hongo wapelekwe kwenye vituo vya kukabiliana na ufisadi na achukukuliwe hatua kali, matatizo haya yataisha.

Hata hivyo,ni muhimu kumhamasisha mwananchi kuhusu haki zake na namna ya kukabiliana na suala la ufisadi. Hali hii inatuonyesha kwamba mipango maalum inapaswa kufanywa na serikali ili kuwaelimisha wananchi kama hatua ya kwanza ya kukabiliana na ufisadi hatimaye izilainishe sekta zote wala si ya uchukuzi pekee .

Maswali

a) Mbali na ajali za barabarani, taja tatizo lingine sugu ambalo linakumba nchi ya Kenya. (alama 2)

***ufisadi***

b) Ajali za barabarani zinasababishwa na nini? (alama 3)

- ✓ ***Zinasababishwa na uendeshaji wa gari kwa kasi sana.***
- ✓ ***Kung'olewa kwa vidhibiti mwendo kinyume na masharti ya uchukuzi na mawasiliano***
- ✓ ***Kuwepo kwa magari mabovu barabarani ambayo hayakutimiza masharti ya ukaguzi***
- ✓ ***Ufisadi wa maafisa wa usalama***
- ✓ ***Barabara mbovu zenye mashimo***
- ✓ ***Matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa madereva wa malori na matrela***

***Hoja zozote 3*1=3***

c) Mwandishi anapendekeza hatua zipi zichukuliwe na serikali ili suluhisho la kudumu lipatikane? (alama 2)

- ✓ ***Wananchi wafahamishwe ya kwamba wana jukumu la kuwawezea walinda usalama endapo gari linapelekwa kwa kasi kupita kiasi***
- ✓ ***Wananchi waelimishwe ili wasikubali kuingia kwenye gari ambalo tayari limejaa kupita kiasi***

***Hoja zozote 2*1=2***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

d) Taja hatua ambazo serikali imechukua ili kuimarisha uchukuzi. (alama 3)

- ✓ ***Kuwekwa kwa vidhibiti mwendo kwenye magari ya abiria***
- ✓ ***Kuwachukulia hatua wale wanaotoa na kupokea hongo***
- ✓ ***Kurekebisha baadhi ya barabara mbovu***
- ✓ ***Kuwekwa kwa mikanda ya usalama kwenye magari***

***Zozote 3*1=3***

e) Ni kitu gani ambacho kinatuonyesha kuwa serikali imeshindwa kukabiliana na ajali za barabarani? (alama 3)

- ✓ ***Kuong'olewa kwa vidhibiti mwendo***
- ✓ ***Kutokuweko kwa mikanda ya usalama***
- ✓ ***Gari kwenda kasi zaidi kutokana na kutojali kwa madereva***

***Zozote 3*1=3***

f) Eleza maana ya maneo haya; (alama 3)

i) tatizo sugu-***shida ambayo imedumu kwa muda bila kupata suluhu ya kudumu***

ii) ukarabati –***urekebishaji***

iii) kuhamasisha-***tia hamu ya kufanya jambo***

**2.UFUPISHO** **(alama 15)**

***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali***

Maelefu ya watu duniani wako hatarani kupoteza maisha yao kwa sababu ya uvutaji wa sigara.Wataalamu wanasema mtu anayevuta pakiti mbili za sigara kwa siku moja ,anapunguza muda wa maisha yake kwa asilimia thelathini.Inaelezwa kwamba ingawa wavutaji wengi wa sigara katika nchi za Ulaya na Marekani wanapunguza au kuacha uraibu huo,wavutaji sigara katika nchi zinazoendelea wanazidi kuongezea kila kukicha.

Kwa muijbu wa wataalamu ,vijana huanza kuvuta sigara kwa sababu ya utundu na kutaka kujua ladha ama mhemko unaosababishwa na sigara. Wengine huanza kuvuta sigara wakifuatisha wacheza sinema maarufu ,wanamuziki au baadhi ya watu wanaowaenzi.

Sigara au tumbaku husababisha athari mbalimbali kwa watumiaji wake ,miongoni mwake yakiwemo magonjwa ya kifua kikuu, kansa ya mapafu ama utumbo na wakati mwingine kifo. Kwa mujibu wa watafiti, watu wanaovuta sigara kwa miaka 20 na zaidi wako hatarini kufa kwa

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

ugonjwa wa kansa ya utumbo.Hii ni kwa sababu moshi wa sigara unaweza kusababisha uvimbe ktika utumbo mkubwa na rektamu.

Uvutaji sigara unachangia asilimia 80-90 ya magonjwa yanayohusiana na kifua ama njia ya hewa ikiwemo kikohozi ,pumu ,homa ya mapafu na kansa ya mapafu. Mvutaji sigara hushambuliwa mara kwa mara na magonjwa ya koo ,mafua na kikohozi kisichokuwa na dawa.

Uraibu huu pia huchangia aslimia 30 ya vifo vinavyosababishwa na magonwa ya moyo.Hewa ya sumu ilioko kwenye sigara huongeza kiasi cha sukari mwlini ambayo huziba mishipa ya damu .Uvutaji sigara husababisha kuta za mishipa za damu zikakamae ; hali ambayo ni hatari na inaweza kusababisha mishipa ya damu ipasuke.Kemikali ya 'nicotene' iliyopo ndani ya sigara inaweza kuongeza shinikizo la damu ,mapigo ya moyo kuongezeka na kupunguza kiasi cha oksijeni kwenye misuli hasa moyo. Mvutaji sigara anaweza kufa ghafla kwani mapigo ya moyo wake yanaweza kusimama ghafla kwa sababu ya shinikizo kwenye moyo wake linalosababishwa na moshi ama kemikali zilizopo kwenye sigara.

Kwa wanawake , uvutaji sigara ni hatari zaidi kuliko kwa wanaume. Mwanamke ambaye anatumia vidonge vya kuzuia mimba na anavuta sigara anaweza kupatwa na athari kubwa za kiafya na kuhatarisha maisha yake. Hatari zinazomkabili ni pamoja na damu kuganda kwa misuli katika sehemu za miguuni na katika moyo. Matatizo hayo yanaweza kusababisha athari zaidi wakati wa ujauzito ama wakati wa kujifungua na hivyo kupelekea mama kufa ghafla kabla ama wakati wa kujifungua.

Kwa mujibu wa utafiti ,watoto wanaozaliwa na akina mama wanaovuta sigara wakati wakiwa wajawazito aghalabu pia wao huanza kuvuta sigara wakiwa na umri mdogo sana. Uvutaji wa sigara kwa mama mjamzito pia huathiri ulimi wa mtoto tumboni na kuwafanya wawe na uzito kuongea ,wazito kujifunza mambo mageni na pia huathiri mapafu yao katika siku zao za baadaye za uhai wao.

Nchini Kenya Serikali imeanzisha mbinu na sheria za kuhakikisha kuwa wavutaji sigara hawavutii katika maeneo ya umma. Sheria hizo zinapiga marufuku uvutaji sigara kwenye maeneo ya umma.Tayari, taasisi mbalimbali za umma na za kibinafsi zimeandika mabango ya kuwaonya wavutaji dhidi ya kuvuta sigara katika mazingira ya taasisi hizo.

Maswali

a) Eleza athari ya uvutaji sigara kwa wanawake .(maneno 25-30) (alama 7)

- ✓ ***Damu kuganda katika mishipa ya miguu na moyo***
- ✓ ***Husababisha matatizo katika ujauzito***
- ✓ ***Ugumu /shida wakati wa kuijfungua***
- ✓ ***Kifo kabla ,wakati au baada ya kuijfungua***
- ✓ ***Huwaathiri watoto na kuwafanya waanze kuvuta sigara wakiwa wachanga***
- ✓ ***Huathiri ubongo wa watoto***
- ✓ ***Huathiri ulimi wa watoto na kuufanya uwe mzito wa kutamka***
- ✓ ***Huathiri mapafu ya watoto***

***Zozote 6 na alama moja ya mtiririko***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

b) Dokeza madhara ya uvutaji sigara.(maneno 45-50) (alama 8)

- ✓ ***Magonjwa kama kifua kikuu –kansa ya mapafu, utumbo***
- ✓ ***Husababisha kifo***
- ✓ ***Moshi wa sigara husababisha uvimbe katika utumbo na rektamu***
- ✓ ***Huleta magonjwa ya kifua –kikohozi kisichoisha, pumu, homa ya mapafu***
- ✓ ***Husababisha magonjwa ya moyo***
- ✓ ***Hukakamaza kuta za mishipa ya damu***
- ✓ ***Huasababisha shinikizo la damu***

***Hoja zozote 7 na alama moja ya mtiririko***

Teacher.co.ke

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

a) Andika neno lenye sifa zifuatazo; kiwamizo sighuna cha ufizi, irabu ya nyuma kati, nazali ya kaakaa gumu na irabu ya chini kati. (alama 2)

***sonya***

Teacher.co.ke

b) Eleza muundo wa silabi katika neno hili (alama 1)

Imeundwa

***i-I***

***me-KI***

***u-I***

***ndwa-KKKI***

c) Andika upya sentensi hii kwa kutumia –o-rejeshi ya kati

Choo ambacho kinachimbwa kimeporomoka. (alama1)

***Choo kinachochimbwa kimeporomoka.***

d) Tunga sentensi zifuatazo; (alama 2)

i) Kiulizo-***Je,kitanda kimetengenezwa***?

ii) Kauli-***Kitanda kimetengenezwa***.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Teacher.co.ke

e. Tunga sentensi moja yenye kiwakilishi cha a-unganifu ,kitenzi kishirikishi kikamilifu na kijalizo (alama 3)

***Cha mwanafunzi kilikuwa kiwanjani.***

f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa. (alama 1)

Kijana yule amekataa jitabu.

***Jana lile limekataa jitabu***.

g) Andika katika usemi wa taarifa; (alama 2)

"Watoto hawa wenu wakicheza hapa watachafua nyumba"Mlezi alisema.

***Mlezi alisema kwamba watoto wao wangeendelea kucheza hapo wangechafua nyumba.***

h) Changanua sentensi hii kwa njia ya jedwali (alama 4)

Tarakilishi nzuri ilikuwa imenunuliwa jana jioni

| S | | | | |
|---|---|---|---|---|
| KN | | KT | | |
| N | V | Ts | T | E |
| ***Tarakilishi*** | ***nzuri*** | ***ilikuwa*** | ***imenunuliwa*** | ***jana jioni.*** |

i) Onyesha yambwa katika sentensi ifuatayo; (alama 3)

Mshali alishonewa suruali na kijakazi kwa uzi mwembamba.

***Suruali-kipozi***

***Mshali-kitondo***

***Kwa uzi mwembamba-shamirisho ala /kitumizi***

j) Eleza tofauti ya kisarufi ya maneno yaliopigiwa mstari . (alama 2)

i) **Kucheka** kwake kulikuwa kwa kipekee.-***nomino***

ii) Mwanaisha anapenda **kucheka** kila wakati.-***kitenzi***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

k. Tunga sentensi kuonyesha wakati ujao wakati ujao hali ya mazoea. (alama 2)

***Mkala atakuwa akiendesha gari.***

l) Tumia neno **paka** katika sentensi kama

m) nomino

***Paka ameyanywa maziwa.***

ii) kitenzi

***Alimpaka*** mafuta kwa mgongo wa chupa.

m) Kwa kutunga sentensi onyesha ngeli mbili za neno **upwa.** (alama 2)

U-U

***Upwa wake Mwanaheri ulimsalimisha mbele ya ami yake.***

U-ZI

***Upwa wa Ziwa Bogoria hauzuruki ikiwa kumejaa maji yaliofurika.***

n) Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii.

Salome alimsimulia Mwakamba kisa chake. (alama 2)

- ✓ ***Kisa kilikuwa cha Salome***
- ✓ ***Kisa kilikuwa cha Mwakamba***
- ✓ ***Kisa kilikuwa cha mtu mwingine***
- ✓ ***Alimsimulia kisa mtu mwingine na kisa cha Mwakamba***
  ***Za kwanza 2*1=2***

o) Rubani nikwa ndege ---***nahodha----------------*** ni kwa meli na ---***dereva----------------*** ni kwa matwana. (alama 2)

p) Tumia alama ya ritifaa katika sentensi kuonyesha matumizi mawili tofauti. (alama 2)

***ung'ong'o-ng'ombe***

***acha silabi-'sema-nasema***

q) Bainisha viambishi katika neno hili (alama 3)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

waliotupiga

***wa-nasfi***

***li-wakati***

***o-kirejeshi***

***tu-nafsi***

***pig-mzizi***

***a-kiishio***

r) unda sentensi yenye muundo ufuatao;

W+V+T+E

**Chake kizuri kimejengwa haraka.**

s) Tunga sentensi yenye kivumishi cha pekee chenye dhana ya kutojali (alama 2)

o-o-te

***Mavazi yoyote yatawafaa.***

**4. ISIMUJAMII (alama 10)**

a) Saiji ya lugha ni nini? (alama 2)

***Ni matumizi ya lugha katika muktadha maalum.***

b) Eleza baadhi ya sifa bainifu za sajili nyingi, (alama 8)

- ✓ ***Msamiati/istilahi zinazotumika –taja msamiati wa sajili hiyo kama vile Sajili ya shuleni***
- ✓ ***Aina za lugha inayotumika –eleza ikiwa inatumia lugha ya amri, upole, vitisho , ukali, udadisi ,lugha ya maswali na majibu, lugha ya kukatiana kauli***
- ✓ ***Adabu katika lugha-eleza ikiwa wazungumzaji huzingatia adabu na kutumia tasfida au lugha ya matusi –zingatia kwa kutoa ithibati***
- ✓ ***Matumizi ya Tamathali za usemi kwa wepesi katika sajili hiyo kama vile tashibihi, maswali balagha, mafumbo, takriri ,methali, kinaya , kejeli nk.***
- ✓ ***Maudhui yanayotawala sajili hiyo***
- ✓ ***Usanifu wa sarufi ya lugha-eleza ikiwa hutumia lugha sanifu au huweza kuvunja sarufi mradi mawasiliano yawepo.-Ikiwa sajili ina sifa hizi mbili ziandikwe zikiwa hija mbili tofauti***
- ✓ ***Urasmi wa lugha-eleza kama lugha inayotamkwa ni rasmi au huweza kuchanganya ndimi***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

- ✓ ***Muundo wa sentensi-eleza sajili hutumia sentensi ndefu ndefu kama vile mahakani au fupi fupi kama vile sokoni-Wakati mwingine sajili inaweza kuwa na miundo hii miwili ya sentensi kutegemea wahusika ,muktadha au kinachozungumziwa .***
- ✓ ***Eleza ikiwa sajili huwa na viziada lugha***

***Hoja zozote 8*1=8***

***Mwisho***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes